

MATAPO YA NYIMBO ZA SHISAFWA

Pendo Mwashota
na
Fokas Nchimbi

Ikisiri

Makala haya yanalenga kuibua mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza katika nyimbo za jamii ya Kisafwa. Mabadiliko yanayoelezwa katika makala haya yamegawanyika katika sehemu kuu mbili. Mabadiliko ya kimaudhui na mabadiliko ya kifani. Katika suala la maudhui, makala yanaeleza kuwa kuna mabadiliko kwa kiasi fulani katika nyimbo za jamii ya Shisafwa tofauti na ilivyokuwa hapo awali kwani watunzi na waimbaji wengi wa sasa wanaelekea kujali zaidi soko na sio ujumbe unaotakiwa kuifikia jamii. Aidha, mabadiliko katika fani yamejitokeza katika vipengele tofautitofauti kama vile uwasilishaji, ushiriki, vifaa, hadhira na madhari. Hali hii inaonesha namna mwingiliano wa kijamii unavyoelekea kuwa na athari katika mambo mbalimbali yanayowazunguka wanajamii husika mpaka katika fasihi yao. Pengine ni kutokana na uhai wa kazi za fasihi yaani kutokuwa tuli kwa sababu kadri jamii inavyobadilika ndivyo na taratibu na mambo mengine yanayoizunguka yanavyobadilika.

1.0 Utangulizi

Makala haya yanaangalia mabadiliko na matapo yanayojitokeza katika nyimbo za Kibantu hususani nyimbo za jamii ya Shisafwa. Jamii ya Wasafwa ina nyimbo za aina nyingi kama vile tumbuizo, tukuzo, chapuzo, na nyinginezo. Nyimbo za jamii ya Wasafwa hasa za zama hizi za kwetu zimesheheni mambo mbalimbali yanayoihusu jamii yenyewe ya Wasafwa na jamii zinazowazunguka Wasafwa na Tanzania kwa ujumla.

Utafiti huu unaonesha kuwa hapo awali nyimbo nyingi za jamii ya Wasafwa zilikuwa zinaimbwa katika miktadha tofautitofauti na kwa lengo maalumu. Hata hivyo, nyimbo nyingi hazikurekodiwa kulingana na hali ya kiuchumi na teknolojia kuwa duni kwa wakati husika. Kwa sasa hali ni tofauti kwa sababu kuna nyimbo za aina mbalimbali na za waimbaji tofautitofauti ambazo zimerekodiwa. Kurekodi huko kumezifanya nyimbo hizo kuenea sehemu mbalimbali nchini Tanzania na nchi za jirani kama vile Zambia na Malawi. Aidha, nyimbo hizi zinaelekea kupendwa na kuwafurahisha wasikilizaji wa aina mbalimbali wa jamii ya Wasafwa na wale wa jamii tofauti. Ukienda kwenye sherehe mbalimbali kama

harusi, ubatizo, kipaimara, komunio, kwenye kampeni za kisiasa, kwenye matambiko, na kwenye sherehe nyingine, utakuta nyimbo zikiimbwa kulingana na miktadha hiyo.

Kuna nadharia mbalimbali ambazo makala haya yangetumia kwa mfano nadharia ya Semiotiki, Uhalisia, Umuundo na nyinginezo. Hata hivyo, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ndiyo iliyotumika. Nadharia hii iliasisiwa miaka ya 1970 na Wolfgang (1974, 1978), Fish (1980) na Tompkin (1980). Hoja kuu ya nadharia hii ni kuwa kazi ya fasihi sio kama sayansi kwamba iwe na jibu moja mahsusi, bali kinyume chake kwa sababu msomaji huwa na mawanda mapana zaidi katika kuichambua kazi husika kwa namna apendavyo Fish (1980). Kwa upande wa Wolfgang (1974) anaeleza kuwa kazi ya fasihi huwa na athari kwa msomaji katika kipindi mahsusi. Kwa mujibu wa mawazo yake ni kwamba kazi ya fasihi huchunguzwa kwa kuangalia mtazamo wa msomaji kuhusu kazi husika ya fasihi. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inakusudia zaidi kumkutanisha msomaji na kazi ya fasihi. Hata maana ya kazi fulani ya fasihi hujiegemeza kwa msomaji wa kazi husika ya fasihi. Wafuasi wa wanadharia hii huamini ya kwamba msomaji wa kazi fulani ya fasihi anaziba mapengo kutokana na maana mbalimbali zinazopatikana katika kazi za kifasihi ambazo ni matokeo ya (a) Kuwepo kwa vipengele lukuki vya kimsingi vinavyounda mwitiko wa msomaji katika matini husika. (b) Kuwepo kwa tofauti kati ya matini husika na mawazo au hisia binafsi za wasomaji wa kazi husika ya fasihi. (c) Matini husika inaweza kuwa tofauti kwa jinsi ambavyo inamuelekeza au kumkanganya msomaji na kupelekea kupata maana tofauti kati ya msomaji mmoja na mwingine.

Suala la tafakari ya kiundani ya kutofautiana kwa maana zinazopatikana katika matini kulingana na mapokeo tofauti ya wasomaji huwafanya wafuasi wa nadharia hii kujiuliza maswali kadhaa kama ifuatavyo:

- (i) Kuna uwiano wowote baina ya maana na kazi ya fasihi inayosomwa au inayosikilizwa na jinsi msomaji au msikilizaji huyo anavyoihakiki?
- (ii) Kila kazi ya fasihi ina maana kulingana na msomaji au msikilizaji binafsi anavyoichukulia?
- (iii) Kuna wasomaji au wasikilizaji wanaofasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wengine?
- (iv) Msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi hutumia vigezo gani kutambua kuwa mawazo yake juu ya kazi fulani ya fasihi anayoichambua yanafaa au

hayafai? Kutokana na maswali hayo, wananadharia wa Mwitiko wa Msomaji wamependekeza mbinu au njia mbili za kuisoma au kuisikiliza kazi ya fasihi. Kwanza ni mbinu ya kuifafanua na kuisisitiza mawazo yaliyojulikana kitambo na kukubaliwa na wasomaji. Pili, ni mbinu ya kuwasilisha kazi ya fasihi kwa kumchochea msomaji au msikilizaji kujitafutia na kugundua mambo mengi katika kazi ya fasihi anayoisoma au kuisikiliza. Katika makala haya mbinu ya pili imetumika zaidi kwa sababu imechochea waandishi wa makala kutafuta na kugundua mambo mbalimbali yanayojitokeza katika nyimbo za Shisafwa suala lililosababisha kubaini suala la matapo yanayojitokeza katika nyimbo hizo.

1.1 Maana ya Nyimbo

Nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mkong'oso, mapigo na muwala. Mwanazuoni huyu anaweka bayana kuwa nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu peke yake au na wazumi wake wakiitikia mkarara (Balisidya 1987:6). Kwa upande wa Mulokozi (1996:64) anaeleza kuwa wimbo ni kila kinachoimbwa. Pia, anasema kuwa wimbo ni dhana pana inayojumuisha tanzu nyingi kama vile tanzu za kinathari kama vile hadithi, huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi zinapoimbwa. Kuna mambo muhimu ambayo yanatambulisha nyimbo, mambo hayo yameelezwa na Mulokozi (1996)

- (a) Muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji
- (b) Muziki wa ala (kama ipo)
- (c) Matini au maneno yanayoimbwa
- (d) Hadhira inayoimbiwa
- (e) Mukstadha unaofungamana na wimbo huo, kwa mfano sherehe, ibada, kilio n.k.

Mulokozi (*keshatajwa*) anafafanua kuwa nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za Kiafrika. Hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuomboleza, kubembeleza mtoto ili alale, kuchapua kazi, kutia hamasa vitani na kadhalika. TUKI (2004:463) wanaeleza maana ya wimbo kuwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Katika makala haya tumefasili maana ya nyimbo kama sanaa yoyote inayotolewa kwa mtindo wa kuimbwa yenye lengo maalumu au lisilo maalumu kulingana na namna mwimbaji alivyoguswa moyoni mwake. Mguso huo unaweza kutokana na mambo mbalimbali yanayomzunguka katika jamii yake kwa wakati anaoishi au wakati aliopitia ambao kwa namna moja au nyingine umeacha athari fulani katika maisha yake. Athari hizo zinaweza kuwa chanya au hasi kulingana na jinsi mtu anavyochukulia atahri hizo.

2.0 Nyimbo za Shisafwa

Wasafwa ni watu wa jamii ya Kibantu wanaoishi katika mkoa wa Mbeya. Kwa mujibu wa Mwakipesile (1975) jamii kubwa kuliko jamii zote katika wilaya ya Mbeya ni Wasafwa. Wasafwa huishi katika milima ya Mporoto Kaskazini ya Mlima Rungwe na katika bonde ambalo laenea kati ya milima ya Mbeya upande wa Kaskazini na milima ya Umalila na Unyiha kwa upande wa Kusini na Kusini Magharibi. Hali kadhalika, Wasafwa huishi upande wa Kaskazini wa mlima Mbeya na katika sehemu ya uwanda wa juu unaopakana na Wilaya ya Chunya. Wasafwa wanazungukwa na jamii hizi:- Wasangu upande wa Kaskazini, Wanyiha upande wa Magharibi, Wamalila upande wa Kusini-Magharibi, na Wanyakusa kwa upande wa Kusini.

Kama ilivyo kawaida kwa jamii mbalimbali duniani kuwa na shughuli tofautitofauti katika maisha, Wasafwa wanajishughulisha na mambo mengi ya kiuchumi na kijamii. Shughuli zao za kiuchumi ni pamoja na kilimo cha mahindi, maharage, mtama, ngano, viazi, na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Pia, Wasafwa wana shughuli nyingi za kijamii. Miongoni mwa shughuli hizo ni harusi, mazishi, matambiko, dini na siasa. Nyimbo kama kipengele cha fasihi, kimekuwa kikitumika sana katika shughuli za kiuchumi na kijamii katika jamii ya hiyo. Nyimbo hizo zinawakilisha maisha yao na uhalisia wa maisha ya kijamii ya kila siku.

2.1 Aina za Nyimbo katika Jamii ya Wasafwa

Jamii ya Wasafwa ina aina mbalimbali za nyimbo kama vile; tumbuizo, tukuzo, chapuzo na nyinginezo. Aina hizo za nyimbo hazitajadiliwa katika makala haya kwa sababu kusudi letu ni kujikita katika kujadili mabadiliko na matapo ya nyimbo za Shisafwa. Kabla ya kujadili matapo ya nyimbo za jamii ya Wasafwa tuangalie kwa ufupi nini hasa maana ya matapo. Matapo ni makundi makuu ya mikondo ya fasihi au sanaa na ya kinadharia yanayotawala nyanja za fasihi au sanaa kwa wakati maalumu na kwa sababu maalumu zinazotokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kijamii, na kiteknolojia ya jamii husika (Senkoro 1987 - msisitizo ni wa maandishi wa makala). Mabadiliko hayo ndiyo yalichangia kwa kiasi kikubwa sana maendeleo ya nyimbo za Shisafwa.

3.0 Maendeleo ya Nyimbo za Shisafwa

Tunapozungumzia maendeleo ya nyimbo za Shisafwa katika makala yetu tuna maana hali ya mabadiliko ya maudhui na fani katika nyimbo za Shisafwa. Mabadiliko ya maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za Shisafwa yanatokana na maendeleo ya jamii kwenye sekta mbalimbali kama vile uchumi, siasa, utamaduni na jamii. Maudhui ya nyimbo za kijadi za Wasafwa ambazo, hasa kwa wakati huo wa kabla ya utandawazi na mageuzi ya kijamii na kiuchumi, zilikuwa ni mali ya

jamii nzima, yalikuwa yanalenga kuburudisha, kuhamasisha, kutia mori, kuonya, kufichua na kuelimisha jamii yote bila malipo katika matukio mbalimbali ya kijamii kwa mfano, sherehe za harusi, kuzaliwa mtoto, wakati wa kazi za kilimo, wakati wa mapambano dhidi ya majanga tofautitofauti na maombi ya mahitaji mbalimbali.

Kwa upande wa mabadiliko ya kifani tumezoea kuona nyimbo za kijadi zikiimbwa kwa kutumia ngoma, filimbi, kayamba wakati mwingine pembe ya ng'ombe imekuwa ikitumika kupigia mbiu kama sehemu ya kunogesha nyimbo za jadi. Pia, mahadhi ya nyimbo za kijadi za Wasafwa yalikuwa na upekee ulioakisi mila na desturi zao, kiasi kwamba hata ukisikia wimbo unaimbwa mahali popote unaelewa tu kuwa wimbo huu ni wa jamii ya Wasafwa. Kwa sasa hivi mahadhi ya baadhi ya nyimbo za Shisafwa yamekuwa ni mchanganyiko wa kijadi na wa kisasa. Mchanganyiko huu unaelekea kutokana na maendeleo ya kijamii, kiuchumi, na kiteknolojia yenye kuchochewa pia na mwingiliano wa kijamii. Kwa ujumla ni vigumu sana kuzuia mwingiliano wa kijamii ambao unatokana na maendeleo yanayosababishwa na miundombinu iliyopo inayoambatana na kukua kwa haraka kwa sayansi na teknolojia.

Vitu kama barabara, televisheni, simu na kompyuta zimerahisisha mawasiliano yanayochochea mwingiliano na mabadiliko ya kiutamaduni na jamii. Kwa hiyo, kutokana na mabadiliko hayo kwa sasa nyimbo za Shisafwa zinaonekana kuwa na mchanganyiko wa ujadi na usasa. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa kwa nyimbo zilizokuwa zinaimbwa kabla ya miaka ya 2000 ambapo sasa hivi kuna matumizi ya vifaa vya kisasa. Nyimbo za Wasafwa zilizoibuka hivi karibuni zimekuwa zikitumia vifaa vya kisasa kama vile; gitaa, kinanda, manyanga, senkamba na kayamba.

Mabadiliko hayo yanahusisha, pamoja na mambo mengine, kubadilika kwa mahadhi ya nyimbo kutoka kwenye ujadi hadi kuelekea kufanana na bongo fleva. Mabadiliko haya yanajidhihirisha pia katika namna ya uimbaji kwa ujumla, vifaa vya mziki vinavyotumika. Hali kadhalika, tukiangalia kwa kina waimbaji wakuu wa aina hizi za nyimbo ni vijana wakati waimbaji wa nyimbo ambazo kwa kiwango kikubwa zimebeba ujadi zaidi ni waimbaji wenye makamo.

Wasanii vijana wa nyimbo za Kisafwa wanaonekana kuathiriwa zaidi na Kiswahili na nyimbo za bongo fleva ambazo zinakua kwa kasi na kusikilizwa na sehemu kubwa ya jamii ya sasa. Nyimbo hizo za bongo fleva kwa kiwango kikubwa sana zinaimbwa kwa lugha ya Kiswahili.

Makala haya yanaonesha kuwa waimbaji vijana wa nyimbo za Shisafwa wameathiriwa na mitindo ya nyimbo za bongo fleva na matumizi ya lugha ya

Kiswahili. Waimbaji vijana wa nyimbo za Shisafwa wamejiingiza kwenye uimbaji wa nyimbo za Shisafwa kwa lengo la kutafuta kipato na kujenga umaarufu. Nyimbo za waimbaji hawa zimesheheni majigambo na malumbano sana kwa sababu ya kuonesha umaarufu na uwezo wa kisanii. Suala hili linajidhihirisha katika wimbo wa *Kadubwidubwi* ulioimbwa na kundi la vijana wanaojiita *Zyomo* ambao wanamwuliza Awilo (mwimbaji maarufu wa nyimbo za Shisafwa) kuwa kwa nini anajiita kidume cha Mbeya. Kundi hilo la waimbaji wanasema kuwa kwani wao ni wanawake? Kwa mfano katika mistari ya kwanza ya wimbo huo inasema:

*“Eheee Nyolinyooo kwa nini eti Awilo anajiita ni kidumee!
Kwani ni kidume kwani wengine sisi ni wanawakee pumbafuu!
Awilo mwingine anajiita Masoksi pumbafuu kwanini Nyolinyo ni
mkali!
Inkhoma isimu igita lili whii?
Ani inkhoma kadubwidubwi!
Inkhoma isimu Awilo uli whii?
Ani ikhoma ikadubwidubwi”*

Tafsiri ya mistari minne ya mwisho

*“Napiga simu Awilo uko wapi?
Mimi napiga kadubwidubwi
Napiga simu gitaa liko wapi
Mimi napiga kadubwidubwi”*

Katika sehemu hiyo ya wimbo wa *kadubwidubwi* tumeona kuwa kuna malumbano baina ya Awilo na kikundi cha waimbaji wanaojiita *Zyomo* kwa sababu ya majisifu ya Awilo ya kujiita kidume cha mbegu cha Mbeya katika albamu yake ya 3. Sehemu inayofuata inaelezea athari mbalimbali za mabadiliko ya nyimbo za Shisafwa kimaudhui.

4.0 Athari za Mabadiliko katika Maudhui

Utafiti huu unaonesha kuwa kwa kiwango fulani nyimbo hizo zenye mwelekeo wa bongo fleva zina mabadiliko kidogo ya kimaudhui. Kwani tukiangalia kwa kina nyimbo za jadi ambazo hazina athari ya bongo fleva zilikuwa zinazungumzia mambo mbalimbali yanayoizunguka jamii ya Wasafwa na jamii iliyo karibu ama jamii nzima ya Kitanzania. Kwa mfano wimbo wa *SIMWANDOJE* unaoitwa *SIMWANDOJE*:

SIMWANDOJE

Usimwandoje na bhana anda yanga weeeX 2!
 Ampela idala na bhana ingaje bhuli nalyooX 2!
 Anda lintesa na bhana anda lintesa weee!
 Ilume nyene bhayayaa anda lintesa weeeX2!
 Ngasiga unanza wee baba ntwale khayaa weeeX 2!
 Ing'ombe zyakho wee baba zili khaya weee!
 Ingaje bhuli ingaje bhuli baba ngaje bhuli nawo!
 Handa antesa na bhana handa ntesa wee
 Handa lintesa na bhuse handa lintesa weee!

Hasa zytutensela untesela ashi
 Idala lyumpela ili kwa kweli lisatosye alele abhana bhundi ibha
 Mbona ifamilya yewa mpela ngosi ini. Nabhuzya nalita wu lume
 wewee
 Uhwendelela antese ampele idala na bhana, ishi izalezi bhamanye
 abhinji
 Aje je Idala lyu mpela na bhana lisitosye alele abhana bhundi saba
 ibha
 Ishi wani akhaa nantwale hu khaya ane!
 Imali zyakho zihwili khaya saga nihalile
 Ihambako ni ndama zihwili khaya ntwale
 Ubaba nu mayi saga bhafwile
 Imbajile avumilile allele abhana saba idala lyumpela ili
 Iga malabha kila pu hwinza khaya uninjilila nalamba ani wani
 akhaaa!
 Sawa ena ndio maisha ndaa Ipole yewempela pasili apole!
 Unume nyene mbona wazidi amateso!
 Umvwi lelo ilintu nyene ahisye lyoli antwale khaya
 Ina maana ababa nu mayi bhe bhalelaje abhana bhakwe bhundi
 saba ibha
 Aga bhalaga na bhana bhakho pampela idala ili
 Leshi ibhukhaje nabho malabho abhana bha ngashe bhakula bhe
 bhayintunza ani
 Womo unyala wa mwene!

KIITIKIO

Usimwandoje na bhana anda yanga weeeX 2!
 Ampela idala na bhana ingaje bhuli nalyooX 2!
 Anda lintesa na bhana anda lintesa weee!
 Ilume nyene bhayayaa anda lintesa weeeX2!

*Ngasiga unanza wee baba ntwale khayaa weeeX 2!
 Ing'ombe zyakho wee baba zili khaya weee!
 Ingaje bhuli ingaje bhuli baba ngaje bhuli nawo!
 Handa antesa na bhana handa ntesa wee
 Handa lintesa na bhuse handa lintesa weee!
 Umwana nyene weee Umwana nyene weeee
 Umwana nyee weee Umwana nyeneee eee
 Handa yanga yoooo Handa yanga weee yooo!
 Mwimbaji: Gubhiligubhili 2007*

TAFSIRI

KIITIKIO

*Simwandoje na watoto anaongea mno
 Ananipa dala na watoto nifanye nini nalo
 Linanitesa na watoto linanitesa mno
 Li mwanaume lenyewe linanitesa sana
 Kama hunitaki nirudishe kwetu
 Sasa nifanyaje nalo
 Kama hunitaki nirudishe kwetu
 Ng'ombe zako wewe baba zipo nyumbani
 Unanitesa sana na watoto wa kupyanga*

*Unachonitesea nini hasaa!
 Dala unayonipa linatosha kulelea watoto wote hawaa!
 Mbona familia uliyonipa ni kubwa hii. Nimekwambia nimechoka
 mwanaume wewe!
 Unaendelea kunitesa kwa kunipa dala na watoto
 Kwa sasa nataka wengi wajue kuwa je dala unayonipa itatosha
 kulelea watoto saba hawa!
 Kwa sasa akhaa! Nipeleke nyumbani mimi
 Mahari zako zipo nyumbani siyo mimi niliyekula
 Ng'ombe dume na ndama zipo nyumbani nipeleke
 Baba na mama hawajafa!
 Nawezaje kuvumilia kulelea watoto saba kwa dala unalonipa!
 Haya ni mateso kila unapokuja nyumbani unaniingilia tafadhali
 akhaaa!
 Sawa haya ndiyo maisha! Pole unayonipa hapajapoa!
 Mme mwenyewe umezidi mateso!
 Msikieni mtu mwenyewe kweli anasisitiza kunipeleka nyumbani!*

*Ina maana wakina baba na mama ndio wawalee watoto wake wote saba hawa!
 Anasema nenda kwenu na watoto na dala analonipa hili!
 Acha tu niende nao hapo baadae wakikua ndio watakaonitunza!
 Mwache tu roho mbaya ni yake
 Sikiyaa sikiyaaa
 Mtoto mwenyewe weee Mtoto mwenyewe weee!
 Ama anasemaa weee Ama anasema yooo weee!*

Wimbo huo unaeleza namna mwanamke mwenye watoto saba anavyomlaumu mume wake kwa sababu ya kumpatia dala (shilingi tano) kwa wakati huo huku watoto ni wengi mno kiasi kwamba hiyo fedha haitoshi. Aidha, katika wimbo tunaona kuwa mume wa Simwandonje anaonekana kuwa ni baba wa familia asiyeijali familia yake kwa sababu ya kutotoa mahitaji yanayotosheleza. Pia, inawezekana yote hayo yanatokana na hali ngumu ya maisha.

Hebu tuangalie mfano wa wimbo ambao ni wa mchanganyiko wa kijadi na wa kisasa. Kwa mfano wimbo wa *Zyomo* unaoitwa ‘*Ayenzile uzyomo*’

AYENZILE UZYOMO (AMEKUJA ZYOMO)

*Lee junior lee junior!
 Ayinzile uzyomo pa Magic Records or lucky junior
 Utungi nu tungi hodi baba mzazi
 Yune mwana wa pa kaya yelaaaa
 Nalambaaa wee Meto mwagona pa sido mwee
 Pachama pa Sowetoo wee!
 Chezsha kibega weee
 Ubhuzye Unambega
 Bhalinda bhavitwa! Bhalinda bhakhanaa
 Ininzile mayii
 Owee ayinzile Uzyomoo
 Ininzile bhayanga
 Bhalinda bhanjanga! Bhalinda bhantelaa!
 Bhasimba zyi nsimba
 Bhahwenya zyhwenya.....*

Wimbo huo wa *Zyomo* umesheheni zaidi sifa za mwimbaji mwenyewe kwa sababu anajisifia kuwa yeye ni mtoto wa nyumbani. Vilevile, wimbo huo unaonesha kabisa kuwa mwimbaji ni wa kizazi kipya tofauti na ule wa Simwandoje kwa sababu mwimbaji anatumia lugha mchanganyiko mara Kiswahili, Shisafwa, Kiingereza na Kinyakyusa. Wimbo huu unaonesha namna mwimbaji huyu

anavyotokea katika jamii ambayo ni mchanganyiko wa jamii tofautitofauti kulingana na mwingiliano.

5.0 Mabadiliko ya Kifani

Katika kueleza mabadiliko ya kifani hapana budi kueleza kidogo maana ya dhana ya fani na umuhimu wake katika uundaji na uwasilishaji wa kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa Wamitila (2010) fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake kwa hadhira lengwa. Vipengele vikuu vya fasihi ya jamii yoyote hubadilika kadri jamii hiyo inavyopitia mabadiliko. Na kama ilivyokwishasemwa hapo awali katika makala hii kuwa jamii ya Wasafwa kama jamii nyingine haijakuwa tuami, bali imekuwa ikipiga maendeleo katika nyanja kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, na kisayansi na teknolojia. Kutokana na maendeleo katika tasnia hizo, pamoja na athari za utandawazi, yametokea mabadiliko makubwa katika kipengele cha fani kwenye nyimbo za Shishafwa. Mabadiliko ya kifani katika nyimbo za Shisafwa yanajidhihirisha katika maeneo kama vile ushiriki, hadhira, mandhari, maleba, na lugha.

5.1 Mabadiliko katika Ushiriki

Hapo zamani washiriki wa nyimbo za Shisafwa walikuwa ni watu walioimba nyimbo na kucheza pamoja na watazamaji. Kwa kuwa malengo na dhima za nyimbo hizo hayakuwa ya kibishara kila mwanajamii alikuwa na uhuru wa kujiunga na kikundi cha nyimbo. Siku hizi kwa sababu ya mabadiliko ya kiuchumi uundaji wa kikundi cha nyimbo za Shisafwa huukiliwa na kuchaguana kunakofanywa na wajasiriamali wa kikundi hicho cha nyimbo. Kwa hiyo, washiriki wa kikundi cha nyimbo za Shisafwa kwa maana ya waimbaji na wachezaji jukwani huundwa na kikundi kidogo cha watu wanaoamua kufanya kazi pamoja wakiwa na malengo ya kujitafutia kipato. Kwa upande mwingine idadi ya washiriki kwa maana ya hadhira ya nyimbo za Shisafwa imeongezeka sana kwa sababu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

5.2 Mabadiliko katika Hadhira

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, siku hizi wanajamii wanaweza kuwa hadhira ya nyimbo za Shisafwa kwa njia ya kutazama moja kwa moja, kuangalia kwa njia ya televisheni, kusikiliza kwa njia ya redio, na kusikiliza kwa njia ya kanda za kaseti. Kwa sababu hiyo hivi sasa si tu Wasafwa wa Mbeya wanakuwa ni wasikilizaji na watazamaji, bali pia watu wa makabila mengine kutoka kila kona ya Tanzania wanaweza kuwa hadhira ya nyimbo za Shisafwa.

5.3 Mabadiliko katika Mandhari

Mandhari ni mahali au eneo linalotumika kutendea shughuli ya kifasihi. Wamitila (*kehatajwa*) anaeleza kuwa mandhari ni mahali wakati wa kihistoria, na mazingira ya kijamii ambayo ni nguzo ya bunilizi au kazi ya kifasihi. Mandhari hayatokei tu bila ya sababu ila huwa ni nguzo muhimu ya kuimarisha matendo ya wahusika, mtazamo uliopo katika kazi inayohusika na usimulizi wenyewe. Hapo zamani waimbaji wa nyimbo za Shisafwa walikuwa wanaimba nyimbo zao zenye malengo na dhima mbalimbali kwenye shughuli za kiuchumi mashambani, kwenye sherehe mbalimbali majumbani, kwenye misiba majumbani, kwenye mashindano ya michezo ya Wasafwa kwenye viwanja vya michezo vya jamii, na kadhalika. Kutokana na maendeleo ya kijamii, kiuchumi, na kiteknolojia mandhari ya nyimbo za Wasafwa yaamebadilika sana. Badala ya kuimbwa kwenye mazingira ya kawaida ya Wasafwa, sasa mandhari ya nyimbo za Kisafwa yanaweza kuwa ni majukwaa ya kisasa kwenye kumbi za muziki au kwenye bar, kwenye kumbi za harusi, na kwenye maeneo mbalimbali ambayo wasanii wa kisasa wa nyimbo za Wasafwa wanaamua kutumia kwa malengo mbalimbali kama vile kwenye mito, kwenye bustani mbalimbali, na kwenye viwanja vya umma.

5.4 Mabadiliko katika Maleba na Vifaa vingine

Hapo zamani wachezaji wa nyimbo za Shisafwa walivaa njuga miguuni, shanga zilizoshonewa kwenye kibwebwe kilichovaliwa viunoni, majani yaliyofungwa viunoni, mikufu iliyovaliwa shingoni, na mavazi mengine yaliyotengenezwa kwa ngozi za wanyama. Vifaa vingine vilivyotumika katika nyimbo za Wasafwa ni pamoja na ngoma, filimbi, pembe za ngombe au nyati, gitaa la kienyeji, manyanga, mapambo ya udongo wa rangi. Wachezaji na waimbaji wa nyimbo za Shisafwa wa zama hizi, pamoja na kudumisha baadhi ya maleba na vifaa vingine vya vya zamani, wanatumia zaidi vifaa vya kisasa zaidi na vifaa vingine ambavyo hapo zamani havikuwapo au ilikuwa ni vigumu kupatikana. Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia vifaa kama gitaa za sasa ni za kisasa zaidi zama hizi kuliko zamani. Hali kadhalika, kuna matumizi ya vifaa ambavyo havikupata kutumika hapo zamani katika nyimbo za Wasafwa. Vifaa hivyo ni kama vile vinanda na piano, trampeti na kadhalika.

5.5 Mabadiliko katika Matumizi ya Lugha

Wasafwa huzungumza Shisafwa. Kwa hiyo katika nyimbo zao walitumia Shisafwa kabla ya watu wengi kujifunza, kuzungumza na kuelewa mambo mengi kwa Kiswahili. Wamitila (*keshatajwa*) anasema kuwa lugha ni kipengele muhimu katika uandishi wa bunilizi na kwa kweli katika fasihi kwa ujumla. Fasihi ni sanaa ya lugha. Kwa hiyo, jinsi lugha inavyotumiwa katika fasihi ni suala muhimu sana katika uchanganuzi wa kazi ya fasihi.

Kuenea na kukua kwa lugha ya Kiswahili kuliwawezesha wasanii wa nyimbo za Shisafwa kutumia lugha hiyo katika uundaji, uhifadhi na uwasilishaji wa kazi zao

ikiwa ni pamoja na nyimbo za Shisafwa. Sababu nyingine iliyoongeza matumizi ya Kiswahili kwenye nyimbo za Shisafwa ni mahitaji ya kupanua soko la kuuza kazi za wasanii hao wa kisasa. Matumizi ya Kiswahili yameongeza hadhira na soko au wateja wa nyimbo za Shisafwa.

6.0 Mjadala mfupi

Katika makala haya tumejadili namna nyimbo za jamii ya Shisafwa zilivyopitia mabadiliko ya kifani na kimaudhui. Mabadiliko hayo yanaelekea kuwa ni matokeo ya suala la maendeleo ya kijamii yanayotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na miundo mbinu bora inayowafanya wanajamii kuchangamana. Mchangamano huo unachangiwa na uibukaji wa mambo mbalimbali ambayo kwa hakika ni matokeo ya sayansi na teknolojia. Hivyo basi vijana au wanajamii wanaweza kutazama nyimbo au wanamuziki kupitia katika luninga zao ama simu za viganjani. Kutazama huko kunawafanya waige baadhi ya mambo ambayo yanafanywa na wanamuziki wa bongo fleva. Matokeo yake wanapotaka kuimba ama kubuni nyimbo za kijamii, hujikuta wakichanganya mahadhi, misimbo n.k suala linalopelekea nyimbo hizo kuwa katikati ya ujadi na usasa tofauti na ilivyokuwa awali. Suala hili linahitaji utafiti wa kina wa athari ya vipengele nyimbo za bongo fleva katika nyimbo za jadi ambao pengine utaibua masuala mengine tofauti na yaliyojadiliwa katika makala haya. Waimbaji wa nyimbo za kijadi u kijamii wanatakiwa kudumisha ujadi katika nyimbo au kazi za kifasihi za jamii husika. Ingawa ni jambo la msingi kudumisha ujadi katika nyimbo za kijamii mwingiliano wa kijamii na upanuzi wa mawanda ya sayansi na teknolojia unaonekana kuwa ni changamoto.

7.0 Hitimisho

Makala yetu yamejadili matapo ya nyimbo za Shisafwa. Katika kuchunguza matapo hayo tumegundua kuwa jamii ya Wasafwa ina nyimbo mbalimbali ambazo zinaelekea kugawika katika makundi. Kundi la kwanza linahusu nyimbo za awali ambazo zilikuwa zinaimbwa na watu wa jamii hii ya Shisafwa. Nyimbo hizi ni zile ambazo hazikurekodiwa bali zilikuwa zinahifadhiwa tu vichwani mwa wasanii. Pia, nyimbo hizi zilikuwa ni mali ya jamii nzima kwa sababu hakukuwa na mmiliki wa kijasiriamali kama ilivyo sasa. Kundi la pili linahusu nyimbo ambazo zimerekodiwa na kundi fulani la watu katika jamii hiyo ya Wasafwa. Nyimbo hizo zinahusu mambo mbalimbali yanayowahusu Wasafwa na wale watu wa jamii inayokaribiana na jamii yao. Nyimbo hizi zinatumia lugha ya Shisafwa tu yaani, hakuna mchanganyiko wa lugha. Kundi la tatu linahusu nyimbo za waimbaji wa kizazi kipya ambao wanadai kuwa wanaimba nyimbo za Shisafwa lakini ukiangalia kwa kina nyimbo zao unakuta aidha zina mwelekeo wa kibongo fleva

au ni mchanganyiko wa Kisafwa na Kiswahili ama ni mchanganyiko wa lugha zaidi ya mbili. Kwa mfano wimbo ufuatao wa *Awilo Masoksi* unaohusu mke wa balozi.

USHI WA BALOZI (MKE WA BALOZI)

*“Nalila weee eee
Nalila weee mama
Mke wa balozi jana alilala londe mayiii
Ushi wa balozi igamo agonile londe mayii
Agonile londe igamo
Yaani mke wa balozi jana alikamatwa ugoni yaani maana yake
alilala nje ya ndoa! Alifumaniwa ugoni. Sasa kesi inageuka hapa
kama mke wa balozi amekamatwa ndugu zangu hii kesi itaenda kwa
nani? Kwa mwenyekiti wa serikali za mitaa au tuipeleke kwa
mtendaji wa kata na tukiipeleka kwa mwenyekiti hii kesi
wanakurudishia kwamba umemwona balozi? Inarudi tena kwa
balozi. Ukihamishia kuipeleka kata wanadai tena tunaomba barua
ya balozi. Sasa balozi utasemaje hapo tunaomba barua sasa mke
wako ndiye aliyelala nje ya ndoa.
Agonile londe mayii
Alilala nje mama
Agonile londe mayii
Alilala nje jana
Agonile londe igamo
Unshi wa balozi undodo
Agonile londe igamo
Mke wa balozi bi mdogo mwee alilala nje jana
Mayi wee mama twalila mama mama
Nalila wee eee, Nalila wee mama
Pole watoto pole, Pole mubhana pole
Pole hwa bhinyu pole, Pole kwa mayi pole
Yaani pole kwa mama pole ,Pole kwa mama pole
Kwa wale wengineo yaani si balozi tu hata watu baki hao yaani
wake zao wanalala nje ya ndoa yaani. Angalieni sana kesi
iliyomkuta balozi.”*

KIITIKIO

*“Mke wa balozi jana alilala londe mayii
Unshi wa balozi undodo agonile londe igamo!”*

Katika wimbo huo wa ‘mke wa balozi’ mwimbaji ameimba wimbo wake kwa kuchanganya lugha mbili yaani, lugha ya Kiswahili na lugha ya Shisafwa. Hata hivyo kwa kiwango kikubwa lugha ya Kiswahili ndiyo iliyotumika zaidi. Hata hivyo sio lengo la makala hii kushughulikia suala la kuchanganya msimbo na kubadili msimbo. Utafiti zaidi unahitajika ili kubaini sababu za kuchanganya msimbo na kubadili msimbo

Marejeo

- Balisdya, N (1987). “Tanzu za Fasihi Simulizi,” Katika *Mulika*, Juz. Na. 9 Uk. 27. Dar es Salaam: TUKI. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Fish, S (1980). *Is there a Text in this Class? The Authority of Interpretive Communities*. Cambridge: Harvard University Press.
- Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mwakipesile, J.S. (1975). “Mila na Desturi za Wasangu, Wasafwa na Wasagara.” Idara ya Utafiti na Mipango, Dar es Salaam, Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana.
- Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Tompkins, J (Mhariri) (1980). *Reader Response Criticism: From Formalism to Post-Structurism*. London: Baltimore.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wamitila K.W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.